Mwaka Wa Yubile

Jioni, marafiki. Nina furaha kuwa hapa usiku wa leo na—na kupata makaribisho hayo mazuri sana, kila mtu anataka ku—kuingia. Inanifanya nijisikie vizuri sana.

2 Si—sijapata nafasi nyingi kuzungumza, ama kusoma, ama chochote kile, kwa maana ibada zangu zote zimekuwa ni uponyaji. Kwa hiyo, napenda tu kuzungumza. Kila mtu anajua hilo. Nadhani mimi . . . Mama alisema niliongea kabla sijatembea. Mnajua jinsi msemo wa zamani ulivyo kuhusu hilo. Kwa hiyo nina furaha sana kujua kwamba Mungu ameubadili moyo wangu, kwamba hayo maongezi yanamhusu Yeye. Mnaona? Nami nataka tu kufa nikizungumza habari Zake, nikiimba sifa Zake na kufanya yale ninayofikiri ni mema.

3 Hatuna muda mwingi sana, kwa sababu tuna ibada ya ushirika usiku wa leo. Jumatano usiku itakuwa ni ibada ya kufundisha, ambapo tutafundisha, Bwana akipenda.

4 Sasa, usiku wa leo, kwa muda mfupi tu, dakika chache, Bwana akipenda, ningependa kuninii . . . Kidogo halitarajiwi, unajua, maana sikuzote ni . . . Naamini Biblia ilisema, "Uwe tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa. Iweni tayari kutoa, au, tayari kutoa jibu kwa habari za tumaini lililo ndani yenu." Na kwa hiyo kama ninaweza kushuhudia kwa habari za tumaini lililo ndani yangu, vema, itakuwa ni baraka kwangu kuwaambia, nami ninatumaini itakuwa ni baraka kwenu kulipokea, na kujua ya kwamba imani yenu inalingana na jambo lile lile. Na tumaini lile lile lililoko ndani yangu, liko ndani yenu, nasi ni raia wenza wa Ufalme wa Mungu.

5 Nilifurahi kusikia juu ya miamsho hii sasa, iko kwenye kanisa la Methodisti huko New Albany. Wala sikusikia kuhusu ule wa huko Louisville, lakini labda mlisikia, ambao Ndugu Fleeman ametwambia hivi punde. Ninyi mlio karibu na miamsho hiyo, ihudhurieni. Ondokeni mwende mpate kuwakilishwa pamoja na watoto wa Mungu, kuonyesha tuko upande gani. Tuko upande wa Bwana, nasi tunataka kuwakilishwa pamoja na watu Wake.

6 Sasa, Jumatano usiku, kama Ndugu Neville alivyosema, ni ibada ya kufundisha. Nafikiri wana namna fulani ya darasa la kufundisha, sivyo, Ndugu Neville? [Ndugu Neville anasema, "Naam."—Mh.] Hiyo ni nzuri sana.

7 Kufundisha Neno daima huliweka Kanisa limeimarika. Tunaishi . . . "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Na asubuhi ya leo tulikuwa tukizungumza juu ya jinsi Neno hilo lilivyokuwa lisiloweza kukosea, jinsi ilivyobidi litimie.

8 Na baada ya wao kuimba, niliwazia, "Vema, nitazungumza juu ya nini?" Basi ikatokea niliwazia, "Lilisema, 'Watakatifu wote watakuwa na Muhuri katika vipaji vya nyuso zao.'" Mnaona? Tutakapofika kule, watakatifu wote watakuwa na Muhuri katika vipaji vya nyuso zao.

9 Nami nikawazia, usiku wa leo, ningesoma sehemu ndogo ya Maandiko kutoka katika Biblia, hapa mahali fulani, na, katika Injili. Basi Yesu, baada ya kumaliza hotuba yake, alisema, "Leo, kwamba, maneno haya *yanatimia*."

10 Sasa, Kristo, katika mwanzo Wake, mwanzo wa huduma Yake; alizaliwa, bila shaka, ulimwenguni, Mwana wa Mungu. Alizaliwa, Yesu Bwana, na kisha baada ya siku nane, za kutahiriwa Kwake, alipewa, sasa, alizaliwa, Kristo Bwana, hasa, naye akapewa Jina la Yesu. *Yesu* lilikuwa "Jina Lake alilopewa." *Kristo* lilikuwa ni "sifa Yake" ya kile alichokuwa. Yeye alikuwa Kristo, Mtiwa Mafuta wa Mungu, alipozaliwa.

11 Na sasa, nikijua kwamba ibada ya ushirika kwa kawaida huchukua muda mrefu kidogo, nami sitaki kuzungumza kwa muda mrefu kupita kiasi, lakini wa kutosha tu, tukihisi Roho wa Mungu amekuja miongoni mwetu, ili tuweze kuwa na i—ibada.

12 Sasa kumbukeni ibada zingine zote ambazo zimetangazwa, miamsho kila mahali, wagonjwa na wahitaji. Yeye alinena nami hivi punde, alipokuwa ametembelea nyumba moja muda mfupi uliopita, ambapo mvulana mmoja, alipagawa pepo, naye alitaka kukombolewa. Sasa, Biblia ilitwambia tu—tukusanyike pamoja na kuwaombea watu hawa.

13 Mnajua, basi, kuna m—msichana mdogo jina lake Georgie Carter ambaye aliponywa, kwa ono, loo, miaka mingi iliyopita. Naye aliondolewa katika kitanda cha mateso ya TB; alikuwa amelala pale kwa miaka minane na miezi tisa, hata hakuwa ameamka kutoka kitandani. Nami nilikuwa. . . nilishuka huko kumwombea. Nami. . . Mnaijua hiyo hadithi, jinsi ambavyo baba na mama hawakuamini katika uponyaji wa Kiungu, na sikukaribishwa sana. Naye huyo msichana alitaka kuponywa.

14 Ndipo siku moja, kule kwa Ndugu Wright, nilikuwa huko nikiwa na i—ibada ya ubatizo, naye huyo msichana alitaka kubatizwa. Wala asingeweza kutoka kitandani, bila shaka. Hakuwa ametoka nje kwa miaka minane au tisa.

15 Nami nilikuwa nikiombea huko nyikani, ama msituni. Ndipo Dada Wright akapiga kengele ili tuje tule chakula cha jioni. Nami nilikuwa nikiomba tu *hivyo*, nao Uwepo wa Bwana wetu Yesu ukiwa karibu sana, hata sikusikia kengele ikilia. Basi giza likaanza kuingia. Ndipo nikaona Nuru ikiangazia chini kwenye kichaka cha miti-mbwa, na kusema, "Shika njia uende kwa Carter."

16 Ndugu Wright, ulikuwa pamoja nami. [Ndugu George Wright anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Basi tulipofika kule, jinsi hasa

lile ono lilivyokuwa limesema, hivyo ndivyo lilivyotukia. Naye Georgie aliponywa mara moja, kutokana na kuwa matesoni miaka tisa na miezi minane, bila kuondoka kitandani. Na hajawahi kurudi kitandani, nijuavyo mimi, isipokuwa awe na mafua ama kitu fulani, mpaka sasa.

17 Nami nasikia kwamba yeye ni mahututi. Tulipokuwa tukifanyia mkutano kwa Ndugu Wright hapa, kabla sijaondoka kwenda nchi za ng'ambo, huyo msichana alikuwa huko juu. Nami ningeweza . . . Nilimwambia Ndugu Wright, baada ya yeye kuondoka, kitu fulani katika Roho wa Bwana kiliendelea kunihimiza kwenda kwa Georgie. Na sasa nasikia kwamba yuko katika hatua ya mwisho ya kansa kwenye titi. Naye alikuwa amekata tamaa, kufa, na alikuwa anaenda kukubali kifo chake.

18 Ndipo akasema ya kwamba alisikia kwamba nimerudi, na, ninamtakia heri, akatoka kitandani, na kusema . . . akaamini angeponywa sasa. Kwa hivyo hiyo ni imani nyingi, mimi . . . kuamini kwamba—kwamba Mungu atasikia maombi ya wanadamu. Kwa hiyo mimi na—na—nampenda Georgie, kama dada yangu. Nami nataka mjiunge nami katika maombi, kwamba Mungu atayaokoa maisha yake. Mimi . . . kama Yeye ataniambia tu la kusema sasa nitakapofika huko.

19 Wengine wengi sana. Bw. Wiseheart, Ndugu Jim Wiseheart aliyekuwa akija hapa, mvulana wa ndugu yake yuko huko hospitalini. Amenipigia simu hivi punde, akiwa na ugonjwa wa Limfu. Huo ni mbaya sana kuliko kansa, mnajua.

20 Nasi tulikuwa na kisa cha huo kuponywa, papa hapa maskanini, hivi majuzi. Mnakumbuka, yule msichana mdogo, daktari alimpa siku thelathini za kuishi; alikuwa mwanafunzi wa shule ya upili hapa. Ndipo mama yake akaja na kumpa Kristo maisha yake na kubatizwa, na huyo msichana, pia. Nao wakasema, "Usimwambie, usimfanye ajue kuwa kifo kiko juu yake." Na kabla ya hapo, akishuka kupitia mstarini hapa, asubuhi hiyo, Roho Mtakatifu alimshika, alijua alichokuwa amefanya, na kadhalika. Naye aliponywa papo hapo, hata wasingeweza hata kupata doa lake. Na hiyo imekuwa kama miaka miwili au mitatu iliyopita. Basi nilikutana na huyo msichana, kama mwaka mmoja uliopita. Nafikiri ameolewa sasa na anaendelea vizuri, hajawahi kuuona tena.

21 Sasa, Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa Limfu. Haileti tofauti yoyote. "Mimi ndimi Bwana niponyaye magonjwa yako yote." Kwa hiyo hebu tuzungumze Naye, kidogo, kwa ajili ya . . . kwa niaba ya wagonjwa, na kwa ajili ya ibada inayoendelea.

22 Sasa, Baba wa Mbinguni mwenye fadhili, kama vile tumekusanyika hapa katika mahali hapa padogo pa kupendeza, labda sio sana kwa macho, kuangalia, lakini, Baba, tunajisikia nyumbani sana hapa, tukijua tu ya kwamba Wewe umetubariki mara nyingi sana. Tunajisikia, mahali hapa padogo, kama

Yakobo, usiku ule, baada ya kumkimbia kaka yake; alivyoona ono, akiwaona Malaika wa Mungu wakipanda na kushuka kwenye ngazi; akayafingirisha mawe pamoja, akasema, "Hii ni nyumba ya Bwana." Baba, ninaomba ya kwamba utawabariki hawa ambao wamekusanyika hapa katika nyumba ya Bwana, usiku wa leo, Betheli.

23 Yasikie maombi yetu kwa ajili ya hawa wagonjwa; yule kijana aliyepagawa na pepo anayemtembelea ndugu yetu.

24 Nasi tunamwombea maskini Georgie, Bwana. Mungu, usiruhusu mauti yammeze. Ulimjalia kuishi, miaka kumi na miwili, kumi na minne sasa, nami ninaomba ya kwamba utaendelea. Wewe Ambaye ungeweza kumtoa TB moja kwa moja, unaweza kumwondolea kansa. Wewe ni Mungu. Nasi tunakupenda, Baba, nasi tunaomba hili kwa imani isiyoyumbayumba.

25 Na pale hospitalini, yule kijana mwanamume, askari kijana amelala pale, akifa, matumaini yote yamekwisha. Lakini, Baba, ilikuwa ni katika saa ya namna hiyo, ulipozungumza na Paulo, ukasema, "Uwe na ushujaa mwingi, Paulo." Nena tena, Bwana. Ninaomba ya kwamba utayaokoa maisha ya huyo mvulana. Lijalie. Naomba asife, Bwana. Naomba aishi, ili utukufu wa Mungu uweze kuletwa katika maisha yake.

26 Tusaidie, usiku wa leo, sasa katika ibada. Utusamehe dhambi zetu. Bila kujua hata neno moja la kusema, tunayakabidhi mambo yote Kwako, na kisha tunaomba kwamba utukufu uwe Kwako, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

27 Sasa, ninapenda tu kuzungumza juu ya Yule tunayemwabudu hapa, Bwana Yesu. Yeye ni mwema sana kwetu, nasi sote tunampenda. Nina hakika, usiku wa leo, kingekuwa kilindi kabisa cha mioyo yetu, kutambua ya kwamba Yeye alikuwa katikati yetu, kama tungeweza tu kumwona Yeye. Lakini Yeye yuko hapa, nitawahakikishia hilo. Kwamba Roho Wake anayeijaza dunia, bahari, na anga, yuko katika ukumbi huu hapa pamoja nasi usiku wa leo. Na Yeye—Yeye, sisi . . . Sifa zetu zinakubalika machoni Pake, Naye anapenda kuabudiwa.

28 Sasa kwa mawazo machache ya kimsingi, juu ya ni kwa nini tuko hapa. Nyumba ya Mungu ni nyumba ya marekebisho. Torati hutoka katika nyumba ya Mungu.

29 Nami nafikiri, katika wakati tunaoishi, na hasa sana katika saa hizi zenye giza nene, baada ya kusafiri na kutazama mataifa yote, kuna tumaini moja tu ambalo ninaweza kuona limesalia, na hilo ni kule Kuja kwa pili kwa Bwana Yesu. Naye hakika atakuja, kama tu alivyokuja hapa mara ya kwanza. Ninaamini hiyo kwa moyo wangu wote, kwa maisha yangu yote.

30 Kwa maana, Neno Lake, kama tulivyoona asubuhi ya leo, halina budi kutimizwa. Ni wazo la Mungu lililodhihirishwa na

Neno Lake, na kufanywa halisi. Tulikuwa na somo asubuhi ya leo, kama baadhi ya wageni, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Sasa, Neno lilikuwa mwanzo. Lakini kabla halijakuwa Neno; Ne—Neno ni wazo lililodhihirishwa. Ilimbidi Mungu kuliwazia kabla hajalifanya kuwa Neno. Ndipo akanena Neno, Nalo likafanyika mwili.

31 Sasa, Yeye yule aliyemtuma Bwana Yesu hapa, kwa Neno Lake lililonenwa, alifanyika mwili akawa Mwana wa Mungu; akafa, kama mtu asiye na hatia kwa ajili ya wenye hatia, ili atukomboe turudi kwenye ushirika na Mungu. Ili sisi, ambao wakati mmoja tulikuwa tumetengwa na Mungu, tuweze sasa kuwa karibu na Mungu, kwa toleo la Damu ya Mwana wa Mungu mwenye haki. Hakika tu kama vile Yesu alivyokuja mara ya kwanza, kama Mkombozi, anakuja mara ya pili kama Bwana-arusi. A—a—anakuja.

32 Na, ingawa, mara nyingi tunawazia, "Vema, ninii . . . Loo, imekuwa muda mrefu. Nasi tumeliwazia hili kwa miaka." Hivyo ndivyo walivyowazia kabla ya Kuja Kwake mara ya kwanza. Nao hawana budi kuwazia jambo lile lile kwa Kuja mara ya pili. Maana, Biblia ilisema kwamba wangesema, "Hakuna tofauti na wakati baba zetu walipolala." Lakini ni katika saa usiyoiwazia, litatukia. Sasa inatupasa . . .

33 Huku Marekani, kama Wakristo Wamarekani, Mungu atahitaji mengi mikononi mwetu, maana tunayo Nuru ya kweli ya Injili na tunashindwa kuitumia jinsi itupasavyo. Kwa hiyo, usiku wa leo, nataka kuzungumza na Mkristo, kuhusu jinsi unavyoweza kuhuzunisha na kumaliza wakati wako wa toba; na jinsi ambavyo ungeweza kutiwa alama kabisa, usiwe na sehemu pamoja na Kristo, kwa kufanya chaguo baya.

34 Sasa, mambo haya kidogo ni makali. Lakini inabidi yawe makali, mara moja moja, ku—kutufanya tumthamini Bwana Yesu.

35 Ndugu mmoja alikutana nami, leo, nilipokuwa nikitoka nje, naye akasema, "Ndugu Branham . . . " Shida za kifedha zimeulemea moyo wake. Akasema, "Baada ya kusikia kuhusu watu maskini huko India, na kadhalika," kasema, "lakini hata hivyo kila wakati . . . " Kasema, "Nina afya njema, na, lakini kila kitu sikuzote kinanisukumia chini."

36 Nikasema, "'Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kurudiwa na Mungu.'"

37 Kila mmoja, inatubidi tu kujaribiwa; mjeledi wa Mungu umewekwa juu yetu, inaonekana kama kutokuwa na hatia. Mungu anafanya hivyo ili kuthibitisha kwamba sisi ni wana. "Wale wasioweza kustahimili adhabu ni watoto haramu," au si wana wa kweli wa Mungu. Lakini mwanamume huyo ama mwanamke anayeweza kusimama na kustahimili kucharazwa

kwao, na kila kitu kikienda kombo, angali anaangalia juu na kusema, "Bwana, nakupenda," huyo ndiye. Yaani, "Yule—yule atakayevumilia hata mwisho, huyo ndiye atakayeokoka." Sasa, ninapenda hilo, sivyo?

38 "Na mkijua neno hili, ya kwamba dhiki huleta saburi; saburi huleta tumaini; tumaini halitahayarishi." Haya basi. Mnaona? "Dhiki huleta saburi." Kuwa na saburi. "Na tumaini halitahayarishi." Nasi tunalo tumaini, usiku wa leo. Katika dhiki zetu zote, bado, inafanya kazi. Dhiki hutufanya tuwe na saburi, tukikungojea Kuja kwa Bwana.

39 "Atakapofunuliwa kutoka Mbinguni mara ya pili, katika utukufu na ukuu, bahari itawatoa wafu wake. Miili iharibikayo ya hao waliolala mauti ndani Yake itabadilishwa na kuwa kama mwili Wake Mwenyewe uliojaa utukufu, ambapo Yeye anaweza kuvitiisha vitu vyote kwa nafsi Yake." Na sisi ni nini, usiku wa leo, ila kuwa Wakristo wenye furaha na kushangilia, tukiitazamia siku ile kuu ya Kuja kwa Bwana.

Yesu, hapa, akinena tena juu ya Neno.

40 Muda mfupi uliopita, kulikuwa na ndugu mpendwa aliyekuja kuniona dakika chache. Huenda akawa humu jengoni sasa. Simwoni. Lakini alisema, "Ndugu Branham, ninalithamini Neno." Ndivyo hivyo, Neno! Neno limethibitishwa. Ndilo jambo ambalo . . . Huwezi kuwa na imani juu ya kitu tu ambacho mtu alisema. Haina budi kuwa na msingi. Basi ni msingi mwingine upi ungekuwa mkuu kuliko Neno la Mungu? Wakati, mbingu zote na nchi zitapita, bali Neno Lake halina mwisho tu kama vile Umilele usivyo na mwisho. Litaendelea mbele zaidi na zaidi, milele litakuwa vile vile. Angalieni, Yesu . . .

41 Kwa kuwa ingetubidi kuharakisha moja kwa moja kwenye andiko sasa, kwa ajili ya ibada ya ushirika. Na hiyo ndiyo sehemu yetu. Kila mwanamume sasa, na mwanamke, mvulana au msichana, anayeliitia Jina la Yesu, itengenezeni mioyo yenu sasa, kwa maandalizi ya meza ya Bwana. Loo, ni jambo la ajabu. Mungu alisema, Yesu Kristo alisema, "Kama wewe . . . Aulaye mwili Wangu, na kuinywa Damu Yangu, anao Uzima wa milele, nami nitamfufua siku ya mwisho. Naye asiyeula, hana shirika Nami. Naye alaye na kunywa isivyostahili, hula na kunywa hukumu kwa nafsi yake." Ni wakati wa jinsi gani! Sasa hebu tujitayarishe kwa ajili ya tukio hili kuu, tukufu, katika dakika chache. Moja wa yaliyo makuu kuliko yote, nafikiri, tuliyo nayo maskanini, ni usiku wa ushirika.

42 Sasa, katika siku za mwanzoni za huduma ya Bwana wetu hapa, Yeye alikuwa amekuja Kapernaumu, nafikiri, tena. "Naye akaketi, kwenye Sabato, hekaluni. Naye mhudumu wa hekalu akampa gombo asome."

43 Mkiangalia, tuna baadhi ya desturi zizo hizo. Yesu, Yeye angesoma Maandiko, kisha awekee msingi mafundisho Yake juu

ya hayo Maandiko. Wakati mwingine ilikuwa ni kinyume na vile Wayahudi walivyodhania ilikuwa, lakini, hata hivyo, ni nani angeweza—ni nani angeweza kumshtaki? Yeye alikuwa ni Bwana wa Utukufu.

44 Naye akasoma Mle ndani ambapo Isaya alisema:

> Amenitia mafuta *kuhubiri mwaka wa Bwana uliokubaliwa.*

45 Ndipo basi alipofanya hivyo, akafunga, na kulikunja hilo gombo, na kuliweka chini; akawageukia watu, akasema:

> *Leo hii* neno *hili limetimia* mbele zenu.

46 Sasa, Isaya, mamia mengi ya miaka, pengine ni kati ya miaka mia tano na mia nane kabla ya hili, alikuwa ametabiri chini ya uvuvio, ya kwamba Kristo, alipokuja, angetiwa mafuta "kuhubiri mwaka wa Bwana uliokubaliwa." Basi ilibidi iwe hivyo hasa, kwa kuwa Mungu, kupitia kwa nabii Wake, alikuwa amenena Neno Lake, nalo Neno Lake halina budi kutimia.

47 Kama tulivyosema asubuhi ya leo, juu ya Isaya, ya kwamba hao watu . . . Ingawa Yesu alifanya mambo mengi makuu mbele zao, hata hivyo, hawangeweza kuamini, kwa sababu Isaya alisema, "Ni nani aliyesadiki habari yetu? Mkono wa Bwana umefunuliwa nani?" Alisema, "Wana masikio lakini hawawezi kusikia, na wana macho lakini hawawezi kuona. Na kwamba wapate kuongoka." Kwa sababu Isaya alisema hivyo, basi hao watu wasingeweza kuelewa hiyo miujiza na mambo ambayo Yesu alikuwa akifanya mbele zao. Je, mnajua, unabii uo huo . . . ?

48 Angalieni, unabii hujirudia. Je, mnajua Maneno ya Mungu yanajirudia, huenda yakizunguka? Kwa mfano, wakati mmoja katika Maandiko, nilisoma kule, na nilikuwa nikijaribu kusoma pambizoni, kote katika Biblia, ambapo ilisema katika Is- . . . katika Mathayo, mlango wa pili, ambapo, ama, mlango wa kwanza, ninaamini, ilisema, ambapo lilitimizwa na Bwana, kwa nabii, "Kutoka Misri nimemwita Mwanangu," akizungumza juu ya Yesu kuitwa kutoka Misri. Pia lilirejea, kwenye wakati Mungu alipowaita Israeli watoke, kwa kuwa Israeli alikuwa ni mwanawe. Nalo Andiko ambalo wao . . . Mathayo alikuwa anarejea, lilikuwa ni Andiko lile lile alilomwitia Mwanawe, Israeli, kutoka Misri, Yeye pia alimwita Mwanawe, Yesu, kutoka Misri. Mnaona?

49 Nayo Maandiko haya, usiku wa leo, tunayosoma Humu ndani, yanatimizwa tena katika siku za Mataifa. "Wanayo macho lakini hawawezi kuona. Wanayo masikio lakini hawawezi kusikia." Naye Mungu anafanya miujiza na ishara na maajabu, nao watu wanalifumbia macho tu jambo hilo, kwa sababu unabii umesema itakuwa hivyo.

50 Sasa, Yesu alitabiriwa, na Isaya, "kuhubiri mwaka uliokubaliwa." Hilo ndilo tunalotaka kushughulikia, usiku

wa leo, sasa. Sasa, "mwaka uliokubaliwa," ulikuwa ni huu, kwamba, mnamo wakati huo, kati ya miaka mingi sana. *Mwaka uliokubaliwa* ni mwaka unaoitwa, katika Maandiko ya Kale, "mwaka wa yubile." Ulikuja kila . . . Naamini ilikuwa ama . . . Kila baada ya miaka saba ilikuwa ni mwaka wa yubile.

51 Na kila baada ya miaka saba waliacha ardhi ipumzike. Hawakukuza tunda lolote juu yake, wala ninii . . . hawakupanda mazao yoyote. Waliacha mazao yao, shambani, yapumzike, kila baada ya miaka saba; na wakati huo ilikuwa ni yubile.

52 Na kila wakati ambapo kulikuwa na mtumwa ambaye alikuwa ameuzwa, au Mwebrania, mtu alikuwa amewauza watoto wake utumwani . . .

53 Sasa, hilo linasikika kama jambo la kuchukiza sana, lakini nilisimama siku chache zilizopita usiku na kuona jambo lilo hilo likitukia. Ambapo, watu wangewaleta binti zao, wasichana, wakawaweka katika soko la watumwa, na kuwavua nguo, na kuwauza huko kama watumwa. Mmoja wa wale jamaa waliokuwamo, si katika kikosi chetu, lakini alikuwa amejiunga nasi pale, alinunua msichana mrembo, kwa jumla ya dola thelathini na tano, na kupata ha—hati katika sheria, kama vile tu unavyopata hatimiliki ya gari. Wengine waliuzwa dola kumi. Wengine walitolewa tu bure. Na jinsi ambavyo, mahali popote ambapo Jina la Yesu Kristo haliheshimiwi, binadamu na wanawake wanakuwa si zaidi ya wanyama.

54 Na jinsi tunavyopaswa kumsifu Mungu kwa ajili ya nchi tunayoishi, kwa maadili na kadhalika. Ni aibu jinsi tunavyochukulia vitu tulivyo navyo, uhuru wa Mungu.

55 Sasa, wangemwuza mtumwa. Kisha huyu—huyu msichana hapa, sasa, anaweza kutoka akawa mke, ama anaweza kuwa kijakazi. Wanamwuza; wanaangalia meno yake, wanaona jinsi alivyo na nguvu, kama anaweza kufanya kazi au hawezi, au kama ni bikira au la, na kadhalika. Nawe unaweza kuwanunua, uwachukue wengi utakavyo, wengi kadiri unaoweza kuwatunza, wengi kadiri uwezao kuwalipia.

56 Na, sasa, jambo lile lile lilikuwa katika siku za Bwana, walipomchukua mtumwa na kumwuza. Basi, kila baada ya miaka saba mwaka wa yubile ulikuja. Sasa, huu ulikuwa ni wakati mzuri sana, nao una maana kuu kwa watu wa siku hizi. Wakati mzuri sana!

57 Sasa, watumwa wangekuwa shambani, au popote walipokuwa, kazini, ndipo labda wameinama chini ya mzigo wa mnyapara, mwenye mali. Naye alikuwa bwana na tajiri wao kabisa, kwa sababu alikuwa na hati rasmi iliyoonyesha kwamba mtumwa huyu ni mali yake. Angemtendea kama farasi, au chochote alichotaka. Alikuwa mtumwa wake.

58 Lakini, basi, kila baada ya miaka saba, ilikuwa ni sheria ya Mungu, ya kwamba kulikuwa na mwaka wa yubile. Basi

mwaka huu wa yubile ulipofika, ndipo kuhani alienda kote nchini, akipiga baragumu, ndipo kila mtumwa aliyenunuliwa kwa gharama, akawa mtumwa, alipewa fursa ya kuwekwa huru, arudi nyumbani tena, kurudi kwa mpendwa wake. Alikombolewa tena, kwa neema. Haikumpasa kulipa chochote. Wapendwa wake hawakupaswa kulipa chochote. Lilikuwa ni tendo la Mungu. Ni kielelezo kizuri jinsi gani!

59 Siku hizi, kwamba wanaume na wanawake, nchini mwetu na popote pale, wamejiuza huko dhambini, kunywa pombe, kucheza kamari, kufanya karamu za ulevi, kufanya mambo wasiyopaswa kufanya, nao wakawa watumwa wa ibilisi. Baadhi . . .

60 Nilikutana na msichana mmoja, hapa si muda mrefu uliopita. Akasema, "Ndugu Branham, ningetoa chochote kama ningeweza tu kuuvunja mnyororo huu wa wiski." Akasema, "Nilianza nilipokuwa msichana mdogo, nikaambatana na mvulana ambaye alikunywa pombe. Tulianza kuchanganya vinywaji, ndipo nikawa mtumwa wake kwelikweli. Nisipoinywa," akasema, "ninaingia tu wazimu. Laiti ningeweza kuondokana na hili!"

61 Nikasema, "Huwezi kulifanya mwenyewe, lakini ninamjua Mtu anayeweza kukuvunjia. Bwana Yesu Kristo amekuja kukuweka huru."

62 Sasa, kama mtaangalia, kwa mfano, mwaka huo wa yubile unajirudia tena sasa. Kila baada ya muda fulani uamsho huipiga nchi; ule uamsho mkuu wa Kiwelshi tu, ulimalizika si muda mrefu uliopita. Hao watu . . . tunaweza kwenda na kuwa na akina Billy Graham na akina Oral Roberts kote nchini, kila mahali. Na haijalishi tunajaribu kiasi gani, jinsi tunavyojaribu sana kuwapanga watu wetu pamoja, na kuwaunganisha, inahitaji Mungu kuleta uamsho. Haijalishi . . .

63 Tunajaribu kuwa na shirika la Wafanyabiashara Wakristo. Hilo ni zuri. Sasa wanajaribu kuwa na shi—shirika la madhehebu mbalimbali. Hayo yote ni mazuri. Lakini, ndugu, maadamu tu ni mwanadamu, kamwe halitakuwa na faida yoyote. Lakini inahitaji Roho wa Mungu kuingia miongoni mwa watu!

64 Sasa katika uamsho huu mkuu wa Kiwelshi ulioanza, huo ulikuwa ni wakati wa yubile kwa watu wa Welshi. Kulitokea, kundi tu la watu wasio na elimu, wakiihubiri tu Injili. Ndipo nguvu na utukufu wa Mungu ukaanza kushuka, hata wafanyabiashara wangeingia kazini na kuketi kwenye dawati lao, na kulia kama watoto wachanga, na kufunga mikuta- . . . shughuli yao. Wakulima shambani wangekuwa wameketi kwenye jembe lao au wakilima. Wangesimamisha ng'ombe wao kuondoka shambani, wenye dhambi kwelikweli, na kuinua mikono yao kwa Mungu, na kulia wapate rehema.

Watu wakitembea barabarani, na kila mahali. Filimbi zikaanza kuvuma, na chochote kile. Uamsho ulikuwa unaendelea.

65 Huo ndio Marekani inaohitaji usiku wa leo. Haihitaji Billy Graham fulani, wala haihitaji Oral Roberts fulani. Inachohitaji, usiku wa leo, ni Roho Mtakatifu akitembea miongoni mwa watu, akidai mwaka wa kuwekwa huru. Hiyo ni kweli. Haihitaji shirika jipya. Haihitaji mpangilio mpya. Kitu pekee inachohitaji ni Roho Mtakatifu kuja katika nguvu za kusadikisha. Unaweza kuhubiri Injili mpaka upate mvi; unaweza kufanya ishara na maajabu mpaka ukaingia mvi; isipokuwa Mungu atoke aingie miongoni mwa watu na kuanza kutenda kazi.

66 Mbona, wakati uamsho huo ulipoanza, mhudumu mmoja alishuka mpaka mahali ambapo palikuwa kalveti iliyovuka barabara. Naye akaipata...akamsimamisha farasi wake, na kuvuka kalveti hii, na kusema, "Mwenyezi Mungu, mji huu umetiwa najisi kabisa huku chini." Kasema, "Mfanye kila mwanamume, mwanamke, mvulana au msichana, anayepitia juu ya kalveti hii, aingie chini ya sadikisho kwa Roho Wako." Akaenda na kumchukua shujaa mzuri, mwaminifu, akamwingiza chini ya mahali hapo, akaombe. Akae mle ndani, mchana na usiku, akifunga, akiomba.

67 Akaingia mjini, na kuomba ruhusa ya kuomba baraka mezani, kabla ya chakula cha jioni kuandaliwa. Wakasema, "Sawa."

68 Naye akasimama na kusema, "Bwana Mungu, sababisha kila mwanaume na kila mwanamke anayeketi kwenye meza hii, apate kusadikishwa."

69 Ndipo ikasemwa, na kuandikwa magazetini, kwamba, "Watu wangepitia juu ya kalveti hiyo, na kuwasimamisha farasi wao barabarani, na kuanza kulia na kuomboleza." "Wanaume na wanawake wangekuja mezani na kuketi na kuchukua chakula chao, na kukisukuma nyuma, nao wangelia na kuomboleza na kutubu."

70 Hiyo ndiyo aina ya uamsho tunaohitaji usiku wa leo, ambapo Mungu anaingia miongoni mwa watu.

71 Tunaweza kuanzisha mkutano, tufanye ishara na maajabu. Ninaliona hapa. Ninatoka nje, na wakati mwingine, katika mkutano, vipofu wanaona, viziwi wanasikia, watu wanakuja na kuangalia, kasema, "Hilo ni ajabu." Huo uamsho ukiisha, hutasikia habari zao tena. Wanarudi moja kwa moja huko nje, "Vema, naam, ninaamini katika hilo."

72 Kinachohitajika, usiku wa leo, si mhubiri mpya. Kinachohitajika ni Roho Mtakatifu, atoke aingie miongoni mwa watu, aanze kuwachochea, wakiona njaa na kiu kwa ajili ya haki. "Heri wao wanapoona njaa na kiu ya haki, maana watashibishwa." Popote ulipo, unahitaji Roho Mtakatifu kuufanya.

73 Sasa, katika siku hizi wakati makuhani hawa... Wangempeleka mtu huyo huko nje, na labda analima kwenye shamba la mahindi; bwana akishuka kule, akimchapa kwa mjeledi, "Harakisha huko! Inabidi uharakishe na hii!"

74 Lakini mara tu baragumu hiyo ilipolia, mtu huyo angeweza kutupa jembe hilo chini, aseme, "Sitalima nalo tena." Ndipo mnyapara yule, mnyapara yule wa watumwa, alikatazwa kumgusa tena, kwa sababu alikuwa huru. Kwa nini? Alikuwa amesikia habari njema. Yubile ilikuwa inaendelea. Upatanisho ulifanywa, ndipo watumwa wote wangeweza kwenda huru.

75 Ninakumbuka, mimi mwenyewe, loo, jamani, niliposikia habari hizo njema zikija moyoni mwangu. Kama mvulana mdogo mwenye dhambi nikiwa nimelala hapa kwenye kitanda cha hospitali, daktari alisema, "Una dakika tatu zaidi za kuishi." Nilisikia sauti kutoka Mbinguni, iliyoniambia mwaka wa yubile ulikuwa unaendelea.

76 Nikamkubali Bwana Yesu, nikafungua pingu zote za dhambi, na kumwambia ibilisi, "Huwezi kunidhuru tena, kwa sababu nimempa Kristo Yesu maisha yangu, wala huwezi kunipiga tena." Tangu wakati huo, amenitishia, mara nyingi. Lakini hajaweza kunigusa tangu wakati huo, kwa sababu yeye ni mwongo tu. Ninaweza kusikia mjeledi wake ukichapa na kucharaza, na kadhalika, lakini haufai kitu. Kwa sababu, hawezi kunipata, kwa sababu mimi ni wa Bwana sasa. Hiyo ni kweli.

77 Sasa tunaona jamaa huyu, baada ya kuwa huru kwenda, alikuwa, kurudi nyumbani kwake, kurudi kwa wapendwa wake, arudi kwa mkewe na watoto wake. Alikuwa huru. Haikumbidi kuwa mtumwa tena.

78 Lakini huu hapa msiba. Ikiwa mtu huyo hakutaka kurudi, naye alitaka kubaki huko, basi bwana huyu alimwendea, kasema, "Unapendelea kuendelea kuwa mtumwa wangu?" "Naam." Basi walimpeleka mpaka hekaluni, wakawatangazia watu, kama ushuhuda wa umma, akaweka sikio lake kwenye mhimili, wakamchoma kwa uma, wakamtia alama sikioni. Basi asingeweza kamwe kuwa huru. Alilazimika kuwa mtumishi maadamu yu hai. Hana budi kuendelea kumtumikia mnyapara huyu wa watumwa, maadamu yu hai, ikiwa alikataa makusudi wito wake na fursa ya kuwa huru.

79 Sasa tulieni wenyewe, kwa muda kidogo tu. Kwa miaka arobaini iliyopita, huku Marekani, sikuzote kumekuwako na mngurumo wa Roho Mtakatifu, akifanya kazi miongoni mwa wanadamu na watu binafsi, akitoa ishara na maajabu, na miujiza ya kila namna. Watu waliobadilishwa, kutoka kwa makahaba, kutoka kwa watu haramu, na kadhalika, na kufanywa waungwana na Wakristo. Kumekuwako na wale ambao wamekuwa vipofu, wamepata kuona kwao. Masikio ya viziwi yamefunguliwa. Wakati mkuu wa yubile kwa wagonjwa

na wanaoteseka, wale ambao wamefungwa na ibilisi! Kwa kila hali, kama amekuwa mgonjwa, kama amekuwa kipofu, kama amekuwa kilema, kumekuwa na maelfu mara maelfu ya miujiza iliyotendwa miongoni mwa watu. Kumekuwa na uamsho unaoendelea daima, makanisani, kwa miaka arobaini iliyopita, wa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na imefikia wakati, kama taifa, na wote, na kama watu binafsi, na kama vikundi vya kanisa, tumeukataa. Tumeondoka na kuukataa.

80 Sasa ubaya wake ni kwamba, marafiki, ukimhuzunisha Roho Mtakatifu mara nyingi sana, basi umevuka mstari wa utengano. Unafikia mahali ambapo hakuna toba iliyosalia kwako, nawe utatiwa muhuri katika ufalme wa giza, ambapo hutawahi kumwona Bwana Yesu. Kamwe hutaona tumaini la Uzima, nawe kabisa utatiwa alama milele. Ni onyo zito jinsi gani! Loo, natumaini Roho Mtakatifu atalizamisha moyoni mwako.

81 Wewe unayesimama mpakani. Wewe ambaye umewazia, mara nyingi, “Ningependa kuwa Mkristo aliyejisalimisha kikamilifu, laiti ningeweza kuamua wakati wa kufanya hivyo.” Loo, ndugu yangu, dada, unatambua ya kwamba hii inaweza kuwa ndiyo nafasi ya mwisho utakayopata ya kuwa hivyo? Huenda ikawa ndio usiku wa mwisho ambao utapata fursa ya kuwa Mkristo mwaminio. Huenda ikawa, tangu usiku wa leo na kuendelea, kwamba umeukataa Ujumbe wa Mungu kwa mara ya mwisho. Ndipo utakuwa, machoni pa Mungu, umetiwa alama katika ukengeufu.

82 Kutakuwa na matabaka mawili tu ya watu katika siku za mwisho. Wote wawili watatiwa alama.

83 Alama ya Mungu ni ubatizo wa Roho Mtakatifu, bila shaka lolote. Nilihubiri hilo si muda mrefu uliopita, papa hapa. Kwa msaada wa Roho Mtakatifu, na Neno la Mungu, nikalithibitisha hilo, ya kwamba muhuri wa Mungu ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Waefeso 4:30 inasema, “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwaye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu.” Bila Roho Mtakatifu, hujatiwa muhuri. Lakini Roho Mtakatifu ndiye Muhuri wa Mungu.

84 Ndipo basi, kwamba, wote ambao hawakutiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu, walitiwa alama ya mnyama. Na alama ya mnyama ni alama ya uasi, ambayo ni, kumkataa Roho Mtakatifu. Mnaona ninachomaanisha?

85 Ndipo wakati mwaka wa yubile, ama mlipuko unapotokea, kwamba watu wanampokea Roho Mtakatifu; nawe makusudi, kwa ukaidi ukamkataa, Mungu hana tena, au, hawajibiki tena kunena nawe tena. Ndipo utatiwa alama, mifano yote ya kale ya Agano la Kale, ni mifano tu na vivuli vya lile Jipya. Na kumkataa Kristo, na kumkataa, ambapo amebisha mlangoni pako, uko kwenye hatari ya kutobolewa sikio. “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu.” Naye Mungu ataweka

kijipazia juu ya masikio yako, hata usiweze kuelewa tena. Nawe hutafanya zaidi ya kuikosoa Injili maadamu uko hai; kisha ufe, na kupotea milele. Ni wakati wa jinsi gani, wakati ungali ni wakati wa yubile, wakati milango iko wazi! Je, ulitambua ya kwamba ubatizo uu huu wa Roho Mtakatifu . . .

86 Nimekuwa nikisoma historia kwa miaka minne, mitano, sita iliyopita, juu ya Roho Mtakatifu, nikijua ya kwamba wakati huu unaonijia sasa, ulikuwa unakuja; kwamba ningeweka kando ibada za uponyaji zisiwe tangulizi, kwa muda, na kuihubiri Injili. Kweli. Jambo la kwanza nililopaswa kufanya . . .

87 Watu walisema, "Kwa nini usifanye *hivi*? Kwa nini usifanye *vile*?"

88 Jambo la kwanza nililopaswa kufanya na karama hiyo ya Kiungu, lilikuwa ni kuivutia mioyo ya watu. Kama sijaishika mioyo yao, wasingesikiliza. Sasa Mungu amelithibitisha, na sasa wananiamini. Wameona mambo ambayo yamesemwa yakitimia, neno kwa neno. Wameona nguvu za Mungu zikitenda kazi sawasawa kabisa. Sasa unachosema, watakiamini. Sasa jambo la kwanza nililopaswa kujua, ni kile nilichokuwa nikizungumzia, kwa kuwa Mungu ataniwajibishia hilo kwenye Siku ya Hukumu. Hiyo ni kweli.

89 Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulishuka, mara ya kwanza tangu Pentekoste, huko Urusi, miaka mia moja iliyopita. Hiyo ni kweli. Hiyo ni historia. Nao walikuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, na wakafanya ishara na maajabu, miaka mia moja iliyopita; kisha wakaukataa, kama taifa, na kuukataa. Basi walipofanya hivyo, wamegeuka sasa wakawa wapinga-Mungu, wapinga-dini, na kuwa wakomunisti, baridi, wenye mioyo ya kikatili. Ikiwa hutamsikiliza Mungu, atakukabidhi kwa roho ambaye atakuhukumu, ugeuzwe uwe aliyeharibikiwa na akili, kuamini uongo na kuhukumiwa nao. Hapo ndipo Urusi inaposimama usiku wa leo, imehukumiwa machoni pa Mungu, kwa sababu ilishindwa kupokea ujumbe wa yubile wa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Waligeuzwa kuwa na akili potovu. Waliamini uwongo, nao wamehukumiwa nao, mbele za Mungu.

90 Mahali pa pili ilipoanguka palikuwa Uturuki, nao Waturuki wakaikataa. Na kusulubishwa, na kutupwa kwenye mabirika, na kadhalika, pamoja na mapanga yaliyochomoza *hivi,* hao Waarmenia, na kadhalika, na kuwaua kwa mamia. Basi angalieni iliko Uturuki usiku wa leo. Ilimpita!

91 Sasa, ndugu yangu, Marekani imekuwa na miaka arobaini ya mahubiri ya kimitume ya mtindo wa kale, mwaka wa yubile. Na kama hawataupokea kama taifa, na ninahofu hawataupokea, ndipo watatiwa muhuri watupwe nje, gizani, ukengeufu mtupu. Madhehebu yetu yote, ni sawa, lakini, ndugu, Mungu haangalii madhehebu. Anaangalia watu binafsi. Ukristo sio dhehebu. Ukristo ni maisha ambayo mtu binafsi anaishi. Amina.

92 Siku moja, ROHO MTAKATIFU ASEMA HIVI kutoka katika Neno la Mungu, kwamba, "Marekani nzima, inamkataa Mungu, na itapokea alama ya mnyama kulingana na Ufunuo mlango wa 13." Na tunaelekea humo. Mungu hawezi kuruhusu taifa lolote . . .

93 Mungu halipendelei taifa. Yeye hawapendelei watu. Anamtaka yeyote atakaye. Na kama taifa moja litachanua na kufanya haya yote na kusimama, milki hiyo ingedumu milele.

94 Lakini kila milki ya ulimwengu itavunjiliwa mbali wakati wa kuja kwa Mwamba uliokatwa kutoka mlimani, bila kazi ya mikono, ambao utavunja falme zote za ulimwengu vipande-vipande. Ndipo Kristo atatawala na kumiliki, na utawala Wake hautakuwa na mwisho. "Naye ataitwa Jina lake, Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele. Na uwezo wa kifalme utakuwa mabegani Mwake, nao huo Ufalme hautakuwa na mwisho." Huo ndio Ufalme wa Mungu utakaokuja kwa nguvu na madhihirisho, lakini ulimwengu mwingine wote utavunjwa na kufarakanishwa. Wataukataa. Mataifa yanaukataa, makanisa yanaukataa, watu binafsi wanaukataa; ili kwamba Mungu aweze kuyahukumu mataifa, aweze kuyahukumu makanisa, aweze kuwahukumu watu binafsi. Kwa maana, mtu anayeifikia ile Kweli, na kushindwa kutembea katika Kweli, basi yeye, kulingana na Maandiko, amemkufuru, au amemkataa, Roho Mtakatifu wa Mungu, akaipita ile Siku ya Ukombozi.

95 Marafiki, mnapozunguka hapa, na vitu mnavyopata . . . Tunavaa nguo nzuri, nguo bora kuliko zote. Watu waliovalia nadhifu zaidi ulimwenguni ni Wamarekani. Watu wanaolishwa vizuri zaidi ulimwenguni ni Wamarekani. Wanaendesha magari bora zaidi ulimwenguni. Wana pesa nyingi kuliko mtu yeyote ulimwenguni. Hiyo ni kweli. Kila kitu tulicho nacho ndicho kilicho bora zaidi ulimwenguni. Tunayo baadhi ya makanisa yaliyo bora sana ulimwenguni. Tuna baadhi ya watu walio bora sana duniani. Na hata hivyo, katika hayo yote, taifa kwa ujumla linamwacha Mungu hatua kwa hatua, kwa sababu tumeliweka juu ya watu binafsi, tumeliweka juu ya madhehebu, tumeliweka juu ya mataifa.

96 Hapa si muda mrefu uliopita, nilimwuliza mtu, nikasema, "Je, wewe ni Mkristo?"

97 Akasema, "Nataka uelewe mimi ni Mmarekani. Mimi ni wa taifa la Kikristo." Vema, hiyo haimaanishi zaidi ya chochote.

Msichana mmoja, nilisema, "Je, wewe ni Mkristo?"

98 Akasema, "Nataka uelewe, ewe kijana mwanamume, ninawasha mshumaa kila usiku."

99 Inaleta tofauti gani unawasha mishumaa mingapi? Inaleta tofauti gani unaishi kiasi gani katika taifa hili? Inaleta tofauti gani wewe ni mfuasi wa kanisa gani? "Mtu asipozaliwa mara ya

pili kwa Roho wa Mungu, hatauona Ufalme wa Mungu." Hilo lilikuwa ndilo jambo la onyo la Bwana wetu Yesu Kristo.

100 Rafiki zangu, hamjui jinsi ninavyowapenda. Hamtambui kwamba wakati mimi. . .kwamba sijaribu kuwakemea kwa sababu tu ninasimama mimbarani; nitakuwa nikiwatumia kwa manufaa yangu.

101 Lakini kile ninachowaambia, usiku wa leo: Onyweni na Injili! Mkimbilieni Kristo! Wekeni kando kila kitu! Usimngoje Binti Jones. Usisubiri uanze kanisani. Uanzishe ndani ya nafsi yako, sasa hivi. Kwa maana wakati unaweza kuja ambapo Mungu atakuelekeza kuwa mtumwa maishani mwako mwote, kwa dhambi ambayo umefungwa nayo kwa muda mrefu. Haijalishi ni gharama gani!

102 Mtu fulani alisema, si muda mrefu uliopita, alisema, "Lakini, Ndugu Branham!" Mtu huyu ni mwaminifu kweli, kile mtu huyo alikuwa akiishi ndani yake, akiishi katika dhambi. "Loo," kasema, "Mimi ni mwaminifu. Ninamwamini Bwana Yesu Kristo."

103 Nikasema, "Ikiwa wewe ni mwaminifu, basi thibitisha kuwa wewe ni mwaminifu. Achana na dhambi unayoishi ndani yake."

"Loo," kasema, "unaona, imehusika sana."

Nikasema, "Nilidhani ulikuwa mwaminifu."

104 Unasema, "Naam, nina *hili* la kufanya. Nina *lile* la kufanya." Jambo la maana sana unaloweza kufanya ni kumjia Yesu Kristo, haijalishi inakupasa kufanya nini. Ni nini muhimu zaidi kuliko—kuliko kuzaliwa mara ya pili?

105 Kila mmoja wenu anajua kwamba siku moja utakuwa fuvu la kichwa na lundo la mifupa iliyolazwa chini ya baadhi ya udongo huu hapa. Kwa hakika tu kama vile unavyoketi hapa usiku wa leo, unaelekea huko. Hiyo ni kweli. Unapaswa kuwa mkweli kiasi gani basi? Unapata ninachomaanisha? Labda unaweza kuanza katika saa moja kuanzia sasa. Wakati huu mwaka ujao, kunaweza kusiwe na hata kipande kimoja cha nyama kwenye mifupa yako, katika miezi kumi na miwili ijayo. Huenda kusiwe na chembe ya uhai mwilini mwako, katika dakika ishirini na tano zijazo. Ndipo basi kuanzia wakati huo, mpaka nyakati zisizo na mwisho zitakapokoma, hautakuwako. Hali unayoingia, hiyo ndiyo hali utakayokuwa milele.

106 Kwa hivyo kama wewe ni vuguvugu, ndugu, hapo ni mahali pa hatari unapoweza kusimama, ni hali ya uvuguvugu. Yesu alisema, "Ama uwe moto au baridi. Ama uwe upande Wangu, kwa moyo wako wote, au uwe dhidi Yangu." Ikiwa utaishi tu maisha mazuri, hayo hayatahesabiwa kamwe. Matambara yenu ya kujiona wenye haki kamwe hayatasimama kwenye Siku ya Hukumu. Hiyo ni kweli.

107 Unasema, “Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa.” Hilo halina uhusiano wowote Nalo. Ninaamini unapaswa kuwa mfuasi wa kanisa, hiyo ni sawa, lakini hilo halina uhusiano wowote na wokovu.

108 Kama tu nilivyosema asubuhi ya leo, huyo mtu alienda kila mahali, akijaribu kumpata Yesu Kristo; tayari alikuwa moyoni mwake. Mambo hayo aliyofanya, kupaza sauti na kunena kwa lugha, na kadhalika, mambo hayo ni sawa, lakini hizo ni sifa za kuonyesha kwamba Kristo yuko mle ndani kwanza. Unaona? Huna budi kumleta Kristo hapa kwanza, ndipo mambo hayo yatatukia. Lakini unaweza kufanya hivyo, bila kuwa na Kristo, halafu basi uko katika matatizo ya namna gani?

109 Sasa, nimeona makafiri wakipiga kelele. Hiyo ni kweli. Nimeona watu wakizunguka na kufanya mambo ya ajabu sana, mpaka ungeweza, unaweza kuamini chochote. Wanamimina kamba kutoka kwenye gunia, namna *hiyo,* wanafanya mazingaombwe fulani juu yake, ndipo hiyo kamba inasimama moja kwa moja hewani. Wanamchukua swila mkubwa, naye anauma, kama ana meno au hana; wanatupa kitambaa huko nje, na kuyaangalia meno yake yakining’inia kwenye hayo matambara. Wanazunguka kule, na kumchezea muziki kidogo, na kuimba, na kumzungushia shingoni mwake. Swila huyo akimtazama tu, anajifanya kama anataka kumuuma, na kisha anaacha. Usimkaribie; atakuua.

110 Nami nimewaona wakisimama pale na kutembea kwenye matuta ya moto, wakati makaa yameteketea. Wanavua walichokuwa wamevaa, wanatembea moja kwa moja kupitia kwenye hayo makaa ya moto bila kufanya lolote, hakuna madhara hata kidogo. Wanaingia kwenye tundu kubwa, lililojaa glasi, na zimechomoza namna *hiyo;* wanakimbia na kufanya mruko mkubwa ndani yake na kulala pale na kujiviringisha tena na tena na tena kisha wanasimama, bila kukatwa kamwe; wanaruka wanatoka. Hiyo ni imani, lakini, ndugu, huo si wokovu. La, bwana. Loo, namna hiyo, njia za ujanja alizo nazo ibilisi za kuwadanganyia watu.

111 Wokovu ni jambo la mtu binafsi na Mungu Mwenyezi, kupitia kwa Yesu Kristo Bwana.

112 Loo, tunachohitaji usiku wa leo, marafiki, ni mmoja wa hiyo mikutano ya mtindo wa kale tuliyokuwa nayo miaka mingi iliyopita, kuenezwa kote nchini. Ambapo, watu walienda nyumbani, wakazinyoosha nyumba zao, wakaondoa ma—maovu nyumbani mwao, wakasitisha upuuzi wao wote nyumbani. Kila nyumba, waliinyoosha vilivyo. Nao wakaachana na uchoyo wao. Waliachana na udanganyifu wao. Wakaachana na uwongo wao. Wakaishi kwa uaminifu na kwa kiasi wao kwa wao; wakaishi kama iwapasavyo Wakristo. Ni dini ya namna hiyo.

113 Na, siku hizi, ninii . . . dini ya namna iyo hiyo tuliyo nayo, imepanuka na kupanuka mpaka ikapambwa karibu ikawa ni maonyesho ya Hollywood. Sasa, mnajua huo ni ukweli. Nasi tunaingia mahali fulani, tunaweka bendi kubwa ya muziki, na kucheza muziki, na kupiga makelele, na kutenda kama, kujifanya, Wakristo. Lakini hebu waendee na kumkaidi mmoja wakati mmoja, ndipo uangalie utakachopata. Unaona?

114 Ukristo ni uvumilivu, wema, upole, unyenyevu, subira. Hiyo ni kweli? "Kristo, aliposhutumiwa, hakushutumu." Hiyo ni kweli? Ukristo ni maisha anayoishi mtu. Ni ujuzi wa kibinafsi. Sio . . .

115 Lakini wengine wanasema, "Kwa hiyo jamaa *huyu*, najua jamaa huyu hufanya *hivi*. Najua anaweza—anaweza kuwaombea wagonjwa nao watapata afya." Hiyo haimaanishi yeye ni Mkristo. Imani itafanya lolote.

116 Na laiti mngelipitia tu mahali pale, kama Wakristo, kundi letu dogo hapa maskanini, ninyi nyote, laiti mngeliona jinsi wachawi na walozi wanavyofanya miujiza. Hakika, wanafanya.

117 Nao wana madhihirisho yote ambayo Ukristo hutoa, lakini hawawezi kuwa Wakristo. Yaangalieni maisha yao, wanayofanya.

118 Watu pale pale hata wanaishi na wanawake wengine, uzinzi, kama dini, nao watu hao hao wanafanya ishara na maajabu. Sio ndani . . .

119 Kuna jambo moja wasiloweza kufanya. Kuna jambo moja tu ambalo sijawahi kuona mchawi yeyote au wowote wale wakifanya. Wanaweza kufanya miujiza, kama vile kufanya kamba hii isimame. Wanaweza kukimbia kupitia motoni, kuuroga huo moto. Nao wanaweza kufanya mambo kama hayo. Lakini hawawezi kuwaponya watu. Hiyo ni ajabu. Wanaweza kuweka laana juu ya watu, nayo magonjwa yatakuja juu ya watu. Lakini hawawezi kuiondoa hiyo laana, na kuwaponya.

120 Imekuwa hivyo kote katika wakati wa Biblia. Wakati Yane na Yambre walipopingana na Musa, wangeweza kuleta vidonda na majipu, ila wasingeweza kuviondoa. Wangeweza kuleta nzi na chawa, ila wasingeweza kuwaondoa. Kwa maana, Bwana Ndiye awaponyaye wagonjwa. Wanaweza kucheza katika roho, nimewaona mara nyingi. Wanaweza kuwa na ujanja wa kila namna, bali hawawezi kuwaponya wagonjwa, au hawawezi kuishi maisha ya Kikristo. Hilo ni jambo moja wasiloweza kufanya.

121 Na hivyo linakuwa jambo la mtu binafsi, kwa kila mwanaume na kila mwanamke. Tunapoona mambo haya yote ya uwongo. Nayo Biblia ilisema, ya kwamba, "Roho hizo mbili zingefanana sana, katika siku za mwisho, hata ingewadanganya walio Wateule kama yamkini." Hiyo ni kweli. "Makristo wa uongo, roho za uongo zikiinuka, zikionyesha

ishara, zikidanganya wengi." Hiyo ni kweli. Lakini, "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu. Mgeni hawatamfuata." Loo, tunaishi katika siku ya jinsi gani! Nao wakati wa yubile unakaribia kufungwa.

122 Sikiliza, rafiki, usiku wa leo, kama uko hapa bila Kristo, wala humjui . . . Una hakika kabisa moyoni mwako, una hakika nalo, bila shaka lolote ya kwamba Kristo yuko moyoni mwako, vema. Lakini ukisema, "Vema, Ndugu Branham, nilivunjika moyo na kulia wakati mmoja nilipokuwa madhabahuni." Usichukue hilo. Unasema, "Vema, nitakwambia, Ndugu Branham, ni—nilikuwa na wakati mzuri, wakati mmoja. Nikacheza katika Roho, kila mahali." Usichukue hilo. Unaona? Unasema, "Vema, nilimwombea mtu fulani, wakati mmoja, akapona." Usichukue hiyo.

123 Jambo unalopaswa kuchukua, ni kujua kwamba wakati Kristo yuko moyoni mwako, majaribu makubwa na shida zinapokuja, Yeye angali ni mtamu kwako. Unatembea vivyo hivyo tu. Ikiwa kila kitu kinaenda kombo, na kila mtu anakupinga, na kila kitu kinageuka hivi, bado wewe ni mtamu na wa kupendeza. Ni sawa. Unasonga mbele moja kwa moja. "Nawe, roho yako, inashuhudia pamoja na Roho Wake, ya kwamba ninyi ni wana na binti za Mungu." Ikiwa hiyo hairudishi mwangwi nafsini mwako, usiku wa leo, rafiki, hebu tusitiwe alama tuondolewe katika Ufalme wa Mungu. Na tuingie katika Ufalme wa Mungu.

124 Na mtu akiisha kutiwa alama katika Ufalme wa Mungu, ametiwa muhuri hadi mwisho wa safari yake. "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa Yeye mmetiwa muhuri hata Siku ya Ukombozi wenu."

125 Sasa, tuna desturi ya mtindo wa kale ya wito wa madhabahuni, kuwaleta watu madhabahuni. Mungu apewe sifa kwa ajili ya hilo. Hilo ni jambo zuri la mtindo wa kale ambalo kanisa la Methodisti lilianzisha miaka mingi iliyopita. Nalo lilikuwa na . . . Lilikuwa zuri; bado ni zuri leo hii.

126 Lakini si lazima uje madhabahuni upate kuwa Mkristo. Hawakuwahi kuwa nayo wakati wa siku za Biblia. Waliwahesabu tu kama waaminio. Hawakufanya wito wa madhabahuni, wakati wote, katika wakati wa mitume, hapakuwapo na wito wa madhabahuni. Walisema, "Wote walioamini walibatizwa." Hiyo ni kweli? Wakawa waaminio.

127 Unaposadiki kabisa kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, na moyoni mwako, sasa, si katika mawazo yako, bali, moyoni mwako, Kitu fulani hurudisha mwangwi huko chini, na kusema, "Sasa nimeokoka," hilo ndilo tu unalohitaji, papo hapo, ndugu. Kiri hadharani, na acha maneno yako yatoke. Ndipo uangalie; angalia maisha yako tangu hapo na kuendelea. Si zaidi ya vile mahindi yangeweza kuzaa gugu, wala

mtu huyo asingeweza kuzaa matunda mabaya. Itambidi kuzaa matunda mema.

128 Yesu alisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Hiyo ni kwa sababu unaamini, sio kuwazia, bali unaamini Hilo. Linakuwa ni wazo moyoni mwako. Jambo linalofuata, ulilionyesha kama maungamo. "Yeye atakayenikiri mbele ya watu, huyo nitamkiri mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu." Kisha kitu fulani kinatia nanga. Huo ndio uhalisi.

129 Lakini yale tuliyofundishwa, rafiki, yametuondoa mstarini. Tumefundishwa, Wamethodisti walifundisha, hapo mwanzo, walisema, "Ndugu, walipofikia mahali wangeweza kupiga kelele, walikuwa na utakaso, walikuwa wameupata wote." Lakini, unakuja kugundua, haikufanya kazi vizuri sana. Hiyo ni kweli.

130 Wakati Wanazarayo wangeweza kupaza sauti, na kuinua mikono yao, wakimbie huku na huku kwenye marefu ya kanisa, walisema, "Huo ndio." Basi wengi wao walipaza sauti na kukimbia huku na huku kwenye marefu ya kanisa, wakatoka na kuishi maisha ya aina yoyote, basi wakajua Hilo silo.

131 Pentekoste ikaja, wakati Mungu alipoanza kuzirudisha zile karama, kanisani, wakaanza kunena kwa lugha. Wakasema, "Huu ndio. Tunao sasa. Tuko tayari kabisa." Lakini wakagundua hawakuwa nao. Hiyo ni kweli. Watu hunena kwa lugha na kuishi maisha ya aina yoyote.

132 Ndugu, jambo ni kwamba, kuwa na hakika! Sasa, kupaza sauti ni sawa. Ninaamini katika utakaso; naam, bwana, si wangu, bali Wake. Unaona? Hiyo ni kweli. Sio utakatifu wangu, bali Wake. Wakati Yeye, Roho Mtakatifu, anapoweka utakatifu Wake humu, ni utakatifu Wake, sio wangu. Mimi ni mwenye dhambi, lakini Yeye ni Bwana.

133 Sasa, ninaamini katika utakaso, naamini katika kupaza sauti, naamini ya kwamba mtu aliyezaliwa mara ya pili atatoa namna fulani ya madhihirisho. Hiyo ni kweli. Ninaamini katika kunena kwa lugha. Ninaamini katika kufasiri lugha. Ninaamini katika kuwaponya wagonjwa. Ninaamini katika kutabiri. Ninaamini katika kufanya miujiza. Lakini mambo hayo yote ni kitu kinachofuata baada ya kumpokea Bwana Yesu Kristo.

134 Kile tumekuwa tukijaribu kusema, "Anapopaza sauti, anao. Anapotabiri, anao." Lakini huo sio alio nao. Kuchuma tofaa mtini, haimaanishi kuwa unao huo mti. Unaona? Una sifa za huo mti. Na hiyo ndiyo imesababisha matatizo. Lakini Kristo anapokolezwa moyoni, mambo haya mengine yote hujitokeza tu yenyewe.

135 Kama sasa inaelekea majira ya kipupwe. Miti yote itapukutisha majani yake isipokuwa mwaloni. Atashikilia majani yake. Majira ya kuchipusha yanapokuja, ni majani ya kale yaliyokufa. Haikubidi kwenda nje na kuyachuma hayo majani kusudi yale mapya yaweze kuchipusha. Acha tu uhai mpya upande juu, ndipo yale ya zamani yatapukutika na mapya yachipuke.

Hivyo ndivyo ilivyo kwa Ukristo.

136 Kumpokea Yesu Kristo, hakuninii. . . Niliwasikia watu wakisema, "Vema, utukufu kwa Mungu, wakati mmoja nililaani. Ningeweza kulaani hata kofia itoke kichwani mwa mtu. Ndipo nikaacha kulaani, ninajua mimi ni Mkristo." Hapana, hujui, kwa njia hiyo. La, bwana. "Wakati mmoja nilikunywa pombe, kisha nikaacha kunywa." Hilo ni jambo jema. Lakini hilo ni jambo adilifu, kwamba *wewe* umeacha hilo.

137 Lakini kumpokea Yesu Kristo ni kuupokea Utu Wake moyoni mwako. Inakufanya uyafie mambo ya ulimwengu, ndipo Kristo anaishi ndani yako. Unaona? Unaweza kabisa kuacha kunywa pombe na bado usiwe Mkristo. Unaweza kuzishika Amri zote Kumi na bado usiwe Mkristo. Kwa maana, kama zile Amri Kumi zingekuokoa, isingemlazimu Yesu kufa. Lakini Yesu alikufa apate kukupa Uzima wa milele. Na hivyo ndivyo ilivyo, ni Roho Mtakatifu anayeishi ndani yako; si kushika sheria ama kufanya mambo, ama kitu kama hicho. Hayo ni matendo. "Huokolewi kwa matendo; bali kwa neema umeokolewa, kwa njia ya imani."

138 Basi kama, moyoni mwako, umempokea Bwana Yesu, una amani Naye. Tazama nyuma, maisha yako. Nitawaambieni aina ya Wakristo ninaopenda kuwaona. Wanapotembea mtaani, wanasema, "Sasa, tazama, unaona jamaa yule anayeenda kule? Sasa, yeye ni Mkristo. Mimi si mfuasi wa kanisa lake, lakini, ndugu, yeye ni Mkristo. Nitakuambia, nimemwona katika matatizo. Unamwona mwanamke yule pale? Naam, bwana. Vema, huenda asionekane maarufu sana miongoni mwa wanawake, lakini yeye ni Mkristo. Nawaambia, yeye ni Mkristo." Jiji zima na liseme, "Yule pale Mkristo." Watajua. Biblia ilisema umetiwa muhuri.

139 Je, umewahi kutia muhuri kwenye kitu chochote? Wanakichukua namna *hii* na kukitia muhuri. Wanaufinya. Uko pande zote mbili.

140 Wanakuona ukija, na kukuona ukiondoka. Hiyo ni kweli? Wewe ni Mkristo, kwelikweli, umetiwa muhuri na Roho wa Mungu. Wanajua ulivyokuwa. Hiyo ni kweli. Ni kushinikiza, kutiwa alama, kutiwa muhuri. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa, hapo ndipo unapotiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu.

141 Kama karatasi hiyo itawahi kutiwa muhuri kisheria, na mthibitishaji rasmi, nalo jina lake limetiwa sahihi juu yake, ni halali maadamu ni karatasi, ndugu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli?

142 Na kama mtu amewahi kuzaliwa kwa Roho wa Mungu, si kujifanya bali kweli amejazwa Roho wa Mungu, amemtia muhuri humo ndani hata Siku ya ukombozi wake. Atakuwa kama Kristo, leo; atakuwa kama Kristo, kesho; atakuwa kama Kristo, kesho kutwa. Katika majaribu, yeye ni kama Kristo; katika matatizo, yeye ni kama Kristo; katika njaa, yeye ni kama Kristo; katika furaha, yeye ni kama Kristo. Kila mahali unapomwona huyo mwanamume ama mwanamke, wanafanana na Kristo, kwa kuwa wametiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu. Mnaona ninachomaanisha? Hiyo si roho yako.

143 Ndugu, dada, usimchezee Mungu muda mrefu kupita kiasi, kwa maana wakati huu unaweza kuja ambapo wakati wa yubile utaupita mlango wako. Kisha utapelekwa kwenye nguzo ya ibilisi, ndipo unatobolewa sikio ndipo huwezi kuisikia Injili tukufu tena. "Unamaanisha nini?" Hutakuwa na haja Nayo. Unajua kumkufuru Roho Mtakatifu ni nini? Ni kumkataa. Hiyo ni kweli.

144 Wakati walipomkufuru Roho Mtakatifu? Walipomkataa Yesu Kristo. Walimwita Beelzebuli. Na kazi zile zile alizokuwa akizifanya, walisema, "Unaifanya kwa Beelzebuli." Yesu akawaambia hao watu, ya kwamba, yale waliyokuwa wamefanya. Hawakuwa wamemwamini, Yeye.

145 Na kama mtu akikataa kuiamini Kweli wakati Kweli imewasilishwa kwake, naye anakataa kuiamini, basi hiyo inalimaliza. Hiyo ni hakika.

146 Kwa hiyo kama humjui Bwana usiku wa leo, si zaidi ya tukio dogo tu ulilokuwa nalo. Ikiwa humjui Bwana kama Mwokozi anayependeza, mwenye fadhili na mwenye upendo; si umjue, usiku wa leo, sasa hivi? Huna haja ya kuja madhabahuni; unaweza ukitaka. Lakini kama humjui . . .

147 Nisikilizeni kwa dakika moja tu, ikiwa nimepata neema machoni penu, kama ndugu yenu, kama mnaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake. Sasa, ninaliweka hili kibinafsi kidogo, lakini ninafanya hivyo kwa sababu fulani. Ikiwa mnaamini kwamba nimekuwa katika uhusiano na Mwenyezi Mungu, kama mnaamini hivyo, nisikilizeni sasa. Usiache jua likuzukie mpaka kitu fulani kimetia nanga moyoni mwako, kwamba wewe ni Mkristo, kwamba uko na amani na adui yako, uko na amani na Mungu.

148 "Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, tuna amani na Mungu kwa njia ya Bwana Yesu Kristo." Warumi 5:1. "Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, tuna amani kwa Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo."

149 Ikiwa una uadui dhidi ya jirani fulani, dhidi ya mtu mwingine ambaye amekudhuru, na mtu huyo amekudhuru; ikiwa wewe, moyoni mwako, huwezi kumpenda mtu huyo, usichukue ujuzi huo. Huna budi kuwapenda wale ambao

hawakupendi. Ukiwapenda wale wanaokupenda, wenye dhambi hufanya vivyo hivyo. Lakini huna budi, sasa, si kutenda tu kana kwamba ni tendo la kidini, bali kutoka moyoni mwako huna budi kufanya hivyo.

150 Nilichowaomba mniombee, hivi majuzi, ama asubuhi ya leo, kwa ajili yangu. Nilifikia mahali nilipowakosoa watu sana, jinsi wanawake wanavyovaa, na mambo kama hayo. Sitaki kuwa hivyo, hayo ni makosa. Sasa ninakiri hilo, papa hapa, kwamba nimekosea. Nami nimewaona wahudumu wakitoka na kufanya mambo yasiyo ya Kimaandiko, nami nasema, "Sasa hayo ni makosa." Mimi ni nani niwahukumu? Mungu ndiye Hakimu wao. Mungu aniondolee roho hiyo. Jalia nifanane na Bwana Yesu. Hiyo . . .

151 Na iwapo . . . hii ni kweli, ndugu yangu, sikiliza, siku moja, siku moja, hutakuwa na fursa ya kuwa kanisani tena.

152 Ninapoondoka na kurudi tena, mke wangu ananiambia, "Unamjua *Fulani-wa-fulani*?"

"Naam."

"Je, ulijua walikufa hivi majuzi?"

153 Hapa, rafiki yangu wa zamani, ambaye nilicheza naye, kama mvulana, Will Edgar King. Yeye ni rafiki msiri wangu, tangu utotoni tukikua. Tumekuwa pamoja. Tulilala pamoja. Tumeishi, tumevua samaki pamoja, kama wavulana wadogo, na kukua. Basi nilipokuwa huko ng'ambo . . . Kijana mwanamume, mdogo, mwenye siha nzuri aliyekuwa ameponywa wakati mmoja, uponyaji wa Kiungu, alikuwa akitembea moja kwa moja kisha akafa papo hapo kwa mshtuko wa moyo. Nani angewahi kuwazia, "Will Edgar King"? Mdogo kuliko mimi kwa yapata miaka minane ama kumi, jamaa mwenye siha nzuri, yapata pauni mia moja na themanini, akitembea, akionekana mwenye afya kabisa; kijana mwanamume mwenye maskini mke mzuri, watoto watatu ama wanne, naye alianguka chini tu. Alikuwa mnunuzi mkuu wa supamaketi zote za kusini. Wadhifa mzuri, nyumba nzuri, familia nzuri, lakini alichukuliwa namna *hiyo*. [Ndugu Branham alidata vidole vyake—Mh.]

Ndugu, Mungu . . . Nafsi yake iko mikononi mwa Mungu mwenye haki ambaye atampa hukumu ifaayo.

154 Tumeketi hapa, usiku wa leo. Mungu pekee ndiye ajuaye tutakuwa wapi asubuhi. Sasa, kama huko sawa na Mungu . . . Tunapoomba, moja kwa moja moyoni mwako sasa; si kwangu, si kwa watu, bali moyoni mwako, mbele za Mungu, sema, "Bwana Yesu, nimekuwa nikicheza tu huku na huku. Lakini, usiku wa leo, ninahisi moyoni mwangu ya kwamba huu ndio wakati ambao ninataka kukukubali Wewe kikamilifu kama Mwokozi wangu. Na tangu sasa na kuendelea, kwa neema Yako, nitaangalia moja kwa moja Kalvari, na kutembea maisha manyofu ya Kikristo."

Na tuombe.

155 Baba wa Mbinguni, ambaye tunampenda na kumwamini, nikijua neno hili, kama mhudumu, kuhani, anayewahudumia watu mambo ya rohoni, nimesimama hapa usiku wa leo kati ya walio hai na waliokufa, nikijua jambo hili, ya kwamba siku moja, bila shaka lolote, itanibidi kuwajibika kwa kila neno, kwenye Kiti cha Hukumu cha Kristo. Nikiwaona wanaume na wanawake humu ndani, watu wa kupendeza, wakifanya chochote ambacho ningewaomba wafanye, Baba. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .nikimwona mtu mhitaji, na mwenye moyo safi. Sasa, Bwana, ni vigumu, kama mwanadamu, pamoja nao, kuleta hayo maneno makali, ya kwamba, hawana budi kumpokea Kristo la sivyo wakataliwe.

156 Baba, hilo linatufanya kujua kwamba nina upendo safi, wa Kiungu kwao, si kitu ambacho kingewadhuru, bali kitu kinachowapenda, Milele. Nami nimewatolea Mwanao, Bwana Yesu, atakayesimama mahali pao kwenye Siku ya Hukumu.

157 Baba, ninaomba ya kwamba utampokea kila mmoja. Kamwe sikuomba mikono iinuliwe. Sikujisikia kufanya hivyo, bali nilihisi kwamba kuna wengi hapa, Baba, wanaotaka kutembea karibu na Wewe. Wanataka kujisalimisha wenyewe, na wanafanya hivyo hivi sasa. Kwa imani, ninaamini hilo, Bwana, ya kwamba sasa wanaweka kando kila mzigo mdogo, na kusema, "Tangu usiku wa leo na kuendelea, kwa kuwa maisha ni dhaifu sana, kwa vyovyote vile, hayana faida sana, nataka kutumia yote niliyo nayo kwa ajili ya Bwana Yesu." Pia, Mungu, jalia kwamba, tangu usiku huu, watatembelea njia hiyo.

158 Halafu basi, Baba, jalia watu hao hao watembee hapa na kula ushirika, usiku wa leo, sasa, mwili uliovunjwa wa Bwana Yesu Kristo. Halafu sisi nasi. . .Wakifanya hivyo kwa moyo mwaminifu, Wewe ulisema utawafufua katika Siku ya mwisho na kuwapa Uzima wa milele. Tujalie mambo haya, Baba mwema, kwa maana tunayaomba katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

159 Sitawauliza ni wangapi waliojiweka wakfu, lakini ninaamini wengi wenu walifanya hivyo. Nami, mwenyewe, nilifanya hivyo moyoni mwangu, "Bwana, niondolee roho hiyo ya ukosoaji."

160 Sasa, siwakosoi watu, mbele ya uso wao, lakini moyoni mwangu huwakosoa. Ninamwona mama mmoja akitembea mtaani, hasa *huyo*, na kuona hajavalia vizuri, nasema, "Hilo si ni baya sana?" Moyoni mwangu; silisemi, kwa mtu mwingine yeyote. Hata hivyo, hiyo ni shauri yake, yeye ana uhuru wa kujichagulia. Yeye hana haki ya kufanya hivyo; Kristo aliyanunua maisha yake; lakini labda haelewi.

161 Kwa hivyo, si kazi yangu kukosoa; acha Mungu afanye hivyo. Ninapokuwa mimbarani, nitahubiri Injili vizuri sana nijuavyo,

na hayo mengine nitayakabidhi kwa Mungu. Bwana awabariki, marafiki.

162 Sasa tutafanya ibada ya ushirika, katika dakika chache tu. Ni wangapi wanaoamini katika ushirika? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Asanteni. Hivyo ndivyo Yesu Kristo alivyotuagiza tufanye, alisema, tule sehemu zilizovunjika za mwili Wake, na tufanye hivyo mpaka atakaporudi tena. Na kama ninyi mnaoamini hii kuwa ni Kweli, na mngependa kuwa na wakati huu mdogo wa ushirika pamoja nasi, karibu na Neno la Mungu hapa, tutafurahi mki—mkikaa pamoja nasi na—na kuwa na wakati huu. Kama sivyo, tutafumukana, katika dakika chache tu. Tungependa mkae pamoja na hao wengine, kwa vyovyote vile, ili mpate kuona jinsi tunavyokula ushirika. Huu sio wa ninii tu . . .

163 Huu ni kwa ajili, pia, kwa ajili ya uponyaji wa Kiungu. Mnajua hilo? Israeli walipokula mfano wake, mwana-kondoo, pasaka, walisafiri miaka arobaini nyikani, nao wakatokea bila hata mtu mmoja aliye dhaifu miongoni mwao. Wazia hilo, pasipo mtu mmoja aliye dhaifu, miaka arobaini. Ushirika, ishara ya waaminio.

164 Sasa, katika Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 11, kuanzia kifungu cha 23, nitasoma hili kwa manufaa ya kanisa. Paulo akizungumza.

> *Kwa maana mimi nimepokea kwa Bwana . . . niliyo . . .* pia *niliyowapa ninyi, . . . Bwana Yesu usiku ule ule . . . aliosalitiwa akatwaa mkate:*
>
> *Na—naye akiisha kushukuru, akaumega, akasema, Twaeni,* na *mle: huu ndio mwili wangu uliovunjwa kwa ajili yenu: fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.*
>
> *Na vivi hivi . . . baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe* hiki ni *cha agano jipya katika damu yangu: fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.*
>
> *Maana kila mwulapo, mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki,* ninyi . . . *mwatangaza mauti ya Bwana hata* ajapo.

165 Je, si ni ajabu hiyo? "Mwaitangaza mauti Yake hata ajapo."

> *Basi kila aulaye mkate huu, na kukinywea kikombe hiki cha Bwana, isivyostahili, atakuwa na hatia ya mwili na damu ya Bwana.*

166 "Je, hii ina maana gani, Ndugu Branham?" Inamaanisha hivi: Ukija na kula ushirika, na kutoka nje na kuishi maisha mengine mbali na yale Mkristo anayopaswa kuishi, unailetea lawama na fedheha huduma ya Bwana Yesu Kristo. Mnalielewa? Ikiwa wewe ni Mkristo, njoo. Ikiwa sio, usije. Tazama.

Lakini mtu ajichunguze mwenyewe, na hivyo aule mkate na kunywa . . . kikombe.

Maana . . . (kifungu cha 29) *Maana alaye na kunywa isivyostahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili wa Bwana.*

Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi *na* dhaifu, . . . *watu kadha wa kadha wamelala.*

Lakini . . . tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa.

Ila tuhukumiwapo, twarudiwa na Bwana, isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia.

167 Tunapokula mkate huu na kukinywea kikombe hiki, na tujichunguze wenyewe, na kusema, "Sasa, je, ninatembea inavyostahili?" Vema, sitembei istahilivyo, la. Lakini Kristo, ndani yangu, ananifanya nitembee istahilivyo. Nampenda. Ninamshuhudia. Mimi si mkamilifu; kamwe sitakuwa, katika ulimwengu huu. Wewe si mkamilifu; kamwe hutakamilika. Lakini upendo wangu Kwake, Naye hunijalia kumwishia, nami ninapenda kufanya hivyo na kumshuhudia Yeye. Sitoki nje na kufanya vituko, na kufanya mambo maovu, ambayo huleta aibu kwa Jina Lake.

168 Kwa maana, nikigundua ya kwamba nimefanya jambo fulani, basi ninarudiwa na Bwana. Kwa nini Mungu afanye hivi? "Isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia."

169 Sasa, kuna tofauti kubwa kati ya mwaminio na asiyeamini. Mungu huwatofautisha.

170 Kumbukeni, waaminio wote huko Misri walikuwa ndani, (Chini ya nini?) chini ya damu. Mwana-kondoo aliuawa. Nayo damu yake ilikuwa imenyunyiziwa mlangoni, kwa hisopo. Angalieni mahali ilipowekwa. "Kwenye kizingiti cha mlango," huo ni mhimili hapa, mwimo. "Kizingiti cha mlango, na kwenye mhimili." Mnaona ni nini? Msalaba, mamia ya miaka kabla ya Mwana-kondoo wa Mungu kuja na kuuawa. Lakini mfano wa Mwana-Kondoo, iliwekwa kwenye kizingiti na mlangoni. Na kila Mwisraeli, akija chini ya damu hiyo, alikatazwa kutoka nje tena. Haya basi, kukatazwa kutoka nje. Walikuwa chini ya damu. Wasingeweza kwenda mpaka amri ilipotolewa ya kuondoka, amri ya kwenda mbele; mfano wa Kristo.

171 "Mara moja, kwa kuwa kwa Dhabihu moja, amekamilisha, milele, wale waliotakaswa katika Kristo Yesu; mara moja, milele." Hakuna kurudi tena, hakuna tena kwenda *hivi,* hakuna tena kufanya *vile.* Loo, utarudi nyuma, ufanye mambo ambayo ni mabaya; tubu tu kisha uje. Unaona? Lakini mara Kristo anapoitakasa nafsi ya mwanadamu, kwa kumjaza na Roho Mtakatifu, imekamilishwa milele. Haya basi, hakuna shauku tena ya kutoka nje. "Maana mwabuduo, akiisha kutakaswa

hana *dhamiri* tena," au, "shauku," tafsiri sahihi. "Mwabuduo, akiisha kutakaswa!" Loo, laiti ningaliweza kuzama ndani hivyo. "Mwabuduo," mwaminio, "akiisha kutakaswa, hana tena tamaa ya dhambi, kamwe." Limetatuliwa milele! "Kwa maana amewakamilisha, kwa Dhabihu moja, hata milele, hao walio katika Kristo Yesu." Ulimwengu unakufa, huujali tena. Unayafikiri mambo yaliyo Juu.

172 Sasa, kama unasema wewe ni Mkristo, na bado unaishi maisha ya kilimwengu, basi unarudiwa na Bwana, kwa maana haikupasi kuhukumiwa pamoja na ulimwengu. "Kwa hiyo, mkutanikapo . . . "

> *Kwa hiyo, ndugu zangu, mkutanikapo mpate kula, ngojaneni.* (Tazama.)
>
> *Mtu akiwa na njaa, na ale nyumbani kwake; msipate kukutanika kwa hukumu. Na hayo yaliyosalia . . .* mimi nijapo *nitayatengeneza.*

173 Mnamwona Paulo hapa. Hao Wakorintho, hawakulipata. Walipanda huko juu, wakala na kulewa katika meza ya Bwana. Nao wanakula na kunywa, wakafanya kila kitu vibaya. Paulo akasema, "Mkutanikapo, akiwa mtu ana njaa, na ale nyumbani kwake. Lakini mkutanikapo, ngojaneni." Kwa maneno mengine, "Subirianeni."

Unasema, "Sasa, huyu hapa ndugu ambaye sidhani kama anapaswa kula ushirika." Vema, usikimbilie kule na kumrusha nje; kuwa na subira naye. Baada ya ibada kwisha, kwa upole, njoo nyumbani kwake usiku fulani na kuketi chini, useme, "Ndugu, mimi . . . Samahani ikiwa nimekosea. Lakini nilikuona hapa chini, hivi majuzi, mtaani, umelewa," chochote alichokuwa akifanya, "huko nje pamoja na mwanamke mwingine ambaye hakuwa mkeo, nawe unakula ushirika. Nakupenda, ndugu. Hebu—hebu mimi na wewe tuombee jambo hili na kuliweka sawa." Mnaona? Ngojaneni. Iweni watumishi ninyi kwa ninyi. Usiwe mkubwa kuliko mtu mwingine. Jaribu kuona jinsi unavyoweza kuwa mdogo.

174 Mara nyingi nimesikia, ikisemwa, "Kamwe usiwe mkubwa machoni pako." Ikiwa wewe ni mkubwa, acha iwe machoni pa Mungu. Kuwa mdogo machoni pako mwenyewe. Kila mtu ajinyenyekezaye, Mungu atamkweza. Lakini wale wanaojikweza, Mungu atawadhili. Mnaona? Iweni wadogo.

175 Mtu huyu anasema, "Vema, yeye ni . . . "

"Vema, najua lakini mimi . . . yeye ni ndugu yangu. Ninapenda kuwa mtumishi wake, mnaona." Iweni watumishi mmoja kwa mwingine. Pendaneni, hivi kwamba, loo, jamani, hata nyinyi—nyinyi . . .

176 Tulizoea kuimba wimbo mdogo. Sijui kama mnaukumbuka sasa. Tungeimba:

Kibarikiwe kifungo kiifungayo
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa nia moja
Ni kama ule wa huko Juu.

Tunapoachana,
Inatuumiza mioyoni;
Lakini tungali tutaunganishwa moyoni,
Na kutumaini kukutana tena.

177 Niliposimama kule chini kwenye makaburi ya Mtakatifu Angelo, na kuyaona yakiwa pale, kote, kwa karibu maili moja, chini ya ardhi, makaburi, ambapo wangelazimika kuwazika wafu wao. Na papo hapo pembeni palikuwa na makaburi madogo madogo, hao walikuwa ni watoto, ambapo waliwaweka watoto pembeni. Na kulikuwako na kanisa dogo kule chini, ambamo iliwabidi kujificha.

178 Nilishuka kule kwenye kanisa kuu la kale la Kirumi ambako waliwachoma kwenye nguzo, wakawalisha simba. Nilitoka pale katikati ya mahali pale, na kusimama pale. Nilitazama pande zote. Nilikuwa sijapaona bado. Uchafu wote uliokuwa umeanguka ndani; na palikuwapo na mahali pakubwa ambapo simba wanatokea. Nikatembea moja kwa moja mahali nilipofikiri labda lile tundu la simba, ambapo Wakristo walifia. Nikainua mikono yangu; nikasimama pale. Nikasema, "Ee Yesu, mimi ni kiumbe asiyestahili, kuwazia kwamba ndugu zangu walitia muhuri ushuhuda wao hapa, kwa vinywa vya simba, na kadhalika, kwa ajili ya huduma ya Yesu Kristo."

179 Ikatokea nilisimama, na kuangalia nyuma yangu, ndipo mtu fulani akauinua msalaba wa kale mchakavu, akisimama kule. Nikaanza kuvumisha moyoni mwangu, "Juu ya kilima mbali sana ulisimama msalaba wa zamani mchakavu, nembo ya mateso na aibu."

180 Jinsi ambavyo watu kote katika nyakati; dunia nzima imelowa damu ya Bwana . . . wafia imani wa Bwana Yesu Kristo. Niliwazia, "Jinsi sisi, tulivyo duni." Unawazia kuhusu kufanya safari ndogo ya umishenari, labda itabidi kustahimili mateso kidogo, mtu fulani akucheke. Ninakuwa mpira wa miguu, hata—hata watu wananichezea sana. Hilo halileti tofauti yoyote. Waliwachezea watu mbele yangu. Walifanya mambo kama hayo, na kuwaita *hiki, kile,* ama *kingine.* Nina Injili ya kuhubiri; nina Bwana ninayempenda; nina lengo la kutimiza. Ndipo nitakapofika mwisho wa safari, nataka kuja, pamoja na kila mmoja wenu nikisema hivi, "Nimevipiga vita vilivyo vizuri."

181 Baadhi ya siku hizi usiku, bila shaka, nitakuwa nimesimama mimbarani, wakati uso wangu utapauka, midomo yangu itafunga, nami nita . . . Sikuzote nimetaka kuvuka mimbara namna hiyo, niende nyumbani Utukufuni. Baadhi ya siku hizi, nitahubiri mahubiri yangu ya mwisho. Nitatoa wito wangu wa

mwisho wa madhabahuni. Nitamwombea mgonjwa wa mwisho. Ninataka kufa nimeshika Biblia mkononi mwangu, nikiliitia Jina la Bwana Yesu Kristo. Nipige vita vilivyo vizuri; nimalize mwendo.

182 Ndugu na dada zangu wapendwa, chochote kilichopo, kama kuna jambo lolote maishani mwako, kinyume na Kristo, hebu na tuliungame, tuje hapa juu sasa tukale meza ya Bwana; tukiiunganisha mioyo yetu kama kitengo kimoja cha imani ya Kikristo, kumfanya Bwana wetu Yesu ajue kwamba tunampenda kwa moyo wetu wote. Mtafanya hivyo sasa tunapoucheza? (Basi, Teddy, tafadhali . . .)

183 Nafikiri wanakuja kwa sehemu. Hiyo ni kweli, ndugu? [Ndugu Neville anasema, "Naam."—Mh.] Sasa kama wazee watajitokeza sasa kutusaidia, na kusimama hapa. Basi unaanzia wapi, ni upande gani, Ndugu Neville, upande *huu*? [Ndugu Neville anajibu.] Vema. Ndugu hawa sasa, wana utaratibu hapa, wa jinsi ambavyo haitatubidi sote kuja mara moja.

184 Na sasa wewe njoo ule ushirika pamoja nasi. Tutafurahi ukija ule ushirika pamoja nasi. [Sehemu tupu kwenye mkanda—Mh.]

185 Nina hakika ya kwamba sote tunaweza kusema, usiku wa leo, kwamba tuna furaha sisi ni Wakristo. Kitendo ambacho tumetenda hivi punde, kina umri wa karibu miaka elfu mbili. Kabla ya kuondoka kwa Bwana wetu Yesu, alituagiza kufanya hivi, na kukifanya hivyo mpaka atakaporudi tena. Naye alitupa hakikisho la Neno Lake Mwenyewe, ambalo haliwezi kushindwa, haliwezi kushindwa kamwe. Alisema, "Aulaye mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu anao Uzima wa milele, nami nitamfufua Siku ya mwisho," Yohana Mtakatifu mlango wa 6.

186 Hilo linanipa tumaini kubwa sana, baada ya kuona dini za uwongo za ulimwengu; kuabudu jua, na kuabudu sanamu, na dhana zao zote za kiumbe cha kimbinguni. Lakini, hata hivyo, kuona Neno hili, jinsi lisivyoweza kukosea! Na Yule Ambaye amethibitisha ya kwamba haliwezi kukosea, ametupa ahadi Yake hii ya Kiungu, kwamba atatufufua katika Siku ya mwisho.

187 Sasa, kwa wageni langoni petu, kuna mengi zaidi kidogo tu kwa hili kuliko yale ambayo tumetoka tu kufanya. Nitayasoma, kwanza, kutoka katika Biblia, katika Yohana Mtakatifu mlango wa 13, kuanzia kifungu cha pili.

> *Hata chakula cha jioni kilipokuwa kimekwisha, ibilisi* ameninii . . . *amekwisha kumtia Yuda Iskariote, mwana wa Simoni, moyo wa kumsaliti;*
>
> *Yesu hali akijua . . . Baba* amempa *vyote* mkononi *mwake, . . . ya kuwa alitoka kwa Mungu, naye anakwenda kwa Mungu;*

Aliondoka *chakulani,. . .akaweka kando mavazi yake; akatwaa kitambaa, akajifunga kiunoni.*

Kisha akatia *maji katika bakuli,* akaanza *kuwatawadha wanafunzi miguu, na kuifuta kwa kile kitambaa alichojifunga.*

Hivyo yuaja kwa Simoni Petro:. . .Petro akamwambia, *Bwana, wewe wanitawadha miguu yangu?*

Yesu akajibu akamwambia, Nifanyayo sasa *wewe hujui. . .; lakini utafahamu baadaye.*

Petro akamwambia, *Wewe hutanitawadha miguu kamwe. Yesu akamwambia, Kama nisipokutawadha, huna shirika nami.*

Simoni Petro akamwambia, Bwana, si miguu yangu tu, bali pia. . .mikono yangu na. . .kichwa.

Yesu akamwambia, *Yeye aliyekwisha kuoga hana* haja ya kutawadha. . .*ila* si *ya kumtawadha miguu yake, bali yu safi mwili wote,. . .mmekuwa safi, lakini si wote.*

Kwa maana alimjua yeye atakayemsaliti; kwa hiyo alisema, *Si nyote mlio safi.*

Basi alipokwisha kuwatawadha miguu, na kuyatwaa mavazi yake, na. . .kaketi tena, akawaambia, Je, mmeelewa na hayo niliyowatendea ninyi?

Ninyi mwaniita, Mwalimu, na Bwana: nanyi mwanena vema; maana ndivyo nilivyo.

Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu; ninyi. . .*imewapasa vivyo hivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi.*

Kwa kuwa nimewapa kielelezo, ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo.

. . .*heri ninyi* mkiyajua mambo haya na *kuyatenda.*

188 Imekuwa ni kanuni ya maskani hii hapa, katika mu—muda wa miaka ishirini na kitu ya kuwepo kwake, kwamba tumekuwa tukifanya zoezi la kutawadhana miguu. Wabaptisti waliiendeleza kabla ya Pentekoste; Pentekoste ikaichukua katika siku zake za mwanzoni; kisha ikaiendeleza. Kwa hiyo sisi, usiku wa leo, kama kawaida tunalizingatia agizo hili.

189 Tuna chumba, hapa, kinachoitwa chumba cha maombi. Wanawake wanaingia humo, kulitekeleza agizo hili kuu ambalo Mungu alituachia.

190 Nao wanaume wanaingia chumbani, kwenye maombi. . . kwenye ofisi hii *hapa,* ofisi ya mashemasi. Nasi tunatekeleza kutawadha miguu.

191 Nawe, mgeni, pamoja nasi usiku wa leo, si mgeni, bali ni raia mwenzetu wa Ufalme, kama hujawahi kutekeleza hili, ama mwanamume au mwanamke, tunakuomba kwa moyo mkunjufu na kukualika uje kujiunga nasi katika ushirika huu. Na kama hujawahi kufanya hivyo hapo kabla, tungefurahi kuwa na ushirika wako usiku wa leo, kwa mara yako ya kwanza, pamoja nasi. Walakini, ikiwa hujisikii kuwa unataka kufanya hivyo, kitu fulani kikikuhimiza uende nyumbani mara moja, ama chochote kile, tunataka kusema ya kwamba tuna furaha ulikuwa hapa pamoja nasi usiku wa leo.

192 Kwa namna fulani ninaomba msamaha kwa kuvunja-vunja mahubiri yangu, na kadhalika, jinsi nilivyofanya, mimi si mhubiri mzuri sana, kwanza kabisa, halafu basi kidogo yanakuja bila kutarajiwa, kidogo inalifanya gumu kwangu. Baadaye kidogo, labda, Bwana atanisaidia katika mambo haya.

193 Na labda baada ya kurudi kutoka huko nje magharibi. . . Natumaini kwamba Bwana atanipa pumziko jema huko nje, ili niweze kurudi, na labda mimi na Ndugu Neville tufanye uamsho mzuri wa mtindo wa kale hapa siku chache usiku, juu ya kufundisha Neno.

194 Kuna mtu fulani, ambaye ndiyo kwanza akutane nami leo, anataka kubatizwa kule mtoni. Ningefurahi kumbatiza mtu yeyote, mahali popote. Ni sawa. Sasa, tuko. . .

195 Sikuzote mumekaribishwa kwenye Maskani ya Branham. Sisi sio dhehebu lolote. Hatuyapingi madhehebu, bali sisi si wa kimadhehebu. Kwa hivyo, sikuzote mumekaribishwa. Hatuna uanachama wowote hapa. Tuna ushirika tu sisi kwa sisi, wakati, "Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, husafisha kutoka—kutokana na udhalimu wote."

196 Na hadi tutakapokutana tena, amani na neema ya Mungu iwe na kila mmoja wenu. Ninaomba kwamba Mungu atawaondolea maradhi miongoni mwenu, na kuwapa safari njema, salama ya kurudi nyumbani usiku wa leo, afya njema na nguvu, nikitarajia kukutana nanyi hapa Jumatano usiku.

197 Hadi wakati huo, neema Yake na iwe pamoja nanyi, tunaposimama tafadhalini. (Mchungaji, chukua. . .) Huyu mchungaji hapa, Ndugu Neville, ataturuhusu tufumukane kwa maombi mafupi.

Mwaka Wa Yubile SWA54-1003E
(Jubilee Year)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili jioni, tarehe 3 Oktoba, 1954, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org